**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME HURU YA FAIFA YA UCHAGUZI**

**JIMBO LA BUCHOSA**

Tarehe 13 Oktoba, 2025

## TAARIFA KWA UMMA
## KUHUSU KUSITISHA UCHAGUZI KATIKA KATA YA NYAKASUNGWA
## JIMBO LA BUCHOSA

Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 71(1) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya mwaka 2024 na kwa barua yenye Kumb. Na. CWS/UCH.02/VOL/32 ya tarehe 10 Oktoba, 2025 kutoka kwa Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Sengerema. Nimepokea taarifa ya kifo cha Ndugu Feruzi Rajabu Kamizula aliyekuwa mgombea wa nafasi ya Udiwani katika Kata ya Nyakasungwa kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM).

Kutokana na kutokea kwa tukio hili. Uchaguzi wa Udiwani katika Kata ya Nyakasungwa, Jimbo la Buchosa Wilaya ya Sengerma Mkoa wa Mwanza umesitishwa kuanzia leo tarehe 10 Oktoba, 2025. Aidha, kwa mujibu wa Kifungu cha 71 (2) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya mwaka 2024, Tume kwa notisi itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali itapanga tarehe nyingine ya uteuzi wa wagombe na taratibu za uchaguzi wa Udiwani katika Kata husika zitaanza upya.

Hivyo, uteuzi kwa wagombea wengine ambao walioteuliwa kihalali utabaki kama ulivyokuwa awali, isipokuwa kama mgombea atajitoa na kwamba hakutakuwa na kampeni kwa wagombea Udiwani katika Kata ya Nyakasungwa mpaka baada ya uteuzi wa mgombea mwingine.

***"KURA YAKO HAKI YAKO JITOKEZE KUPIGA KURA"***

Imetolewa na:

Deogratius C. Lihengelimo
**MSIMAMIZI WA UCHAGUZI**
**JIMBO LA BUCHOSA**

TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI
MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
JIMBO LA BUCHOSA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUCHOSA

UCHAGUZI MKUU OKTOBA 29, 2025
Kura Yako Haki Yako Jitokeze Kupiga Kura

S.L.P 44, BUCHOSA-SENGEREMA, Simu +255 (026) 2963630, Nukushi +255 (026) 2963629,
Barua pepe: ded@buchosadc.go.tz, Tovuti: www.buchosadc.go.tz